

Ufugaji wa bata wa mayai

Ufugaji wa bata ni maarufu sana na ni biashara yenyе faida kubwa kabisa. Kuna aina nyingi za bata wa nyama na mayai ulimwenguni kote.

Bata wote waliopo duniani kote hutoka kwa ndege wa porini. Ndege hao wa porini hutangatanga duniani kote na baadhi yao wamefugwa kama chanzo kizuri cha chakula. Maelfu ya bata wanaweza kufugwa bila maji kwa kuwaweka ndani ya banda jinsi unavyofuga kuku. Endapo utafuga bata bila maji, bata wako watataga mayai ambayo hayajarutubishwa. Mayai haya hayataanguliwa kwa ajili ya kuzalisha vifaranga. Bata dume na maji ni muhimu kwa ajili ya kuzaliana au kupandana.

Usimamizi

Bata wanaweza kufugwa kibiashara na kwa kiwango kidogo kwa ajili ya uzalishaji wa nyama na mayai. Bata huhitaji makazi ya gharama nafuu, rahisi na yasiyo ya kifahari, na hivyo basi gharama ya chini ya kuanzisha biashara ya ufugaji wa bata. Bata ni ndege sugu sana na wanahitaji usimamizi mdogo.

Bata wanaweza kuzoea kila aina ya hali ya mazingira wenyewe. Wanaweza kutaga mayai usiku au asubuhi. Unahitaji nafasi kidogo kwa ufugaji wa bata.

Faida

Bata wana kipindi kifupi cha kutaga na kuangua vifaranga. Vifaranga hukua haraka, na ni sugu sana dhidi ya magonjwa ya kawaiida ya ndege. Unaweza kulisha bata wako na aina mbalimbali za vyakula vinavyojumuisha; mihogo, mahindi, mpunga, matunda na vyakula vingine vya bei nafuu na vinavyopatikana kwa urahisi.

Pia bata wana tabia ya kutafuta magugu majini, mwani, kunde kijani, minyoo na wadudu mbalimbali ambao hupunguza gharama ya chakula. Bata wana kiwango kidogo cha vifo na hutaga mayai kwa muda mrefu.

Faida nyingine

Bidhaa za bata kama vile nyama na mayai zina mahitaji makubwa katika soko la ndani na kimataifa, kwa hivyo ni chanzo kikubwa cha mapato na ajira.

Bata aina ya indian runner aina maarufu sana kwa ajili ya uwezo wao wa kuzalisha mayai. Kuna aina tatu za bata wa indian runner zinazopatikana. Bata aina ya indian runner nyeupe na kijivu ni bora kwa uzalishaji wa mayai. Bata aina ya corky campbell pia maarufu sana kwa uzalishaji mkubwa wa mayai.